

NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

25 Novemba 2021

Kwa Marafiki Waliokusanyika katika Nchi
Takatifu Kuashiria Maadhimisho ya Miaka
Mia Moja ya Kupaa kwa ‘Abdu’l-Bahá

Mioyo yetu imejawa na mshangao tunapotafakari umuhimu wa tukio hili la maana sana: kukamilika kwa miaka mia moja tangu kufariki kwa ‘Abdu’l-Bahá, miaka mia moja tangu kuanza kwa Zama za Ujenzi za Kipindi cha Kibahá’í na miaka mia moja tangu Imani ya Bahá’u’lláh ilipokabidhiwa kwa Utaratibu Wake wa Kiutawala, ambayo asasi zake ndizo mnaziwakilisha hapa. Ni la kushangaza jinsi gani Agano Lake, ambalo kupitia hilo “Mfumo huu wa kipekee, huu wa ajabu” umeanzishwa katika mataifa yen una michakato yake kufanywa ifanye kazi. Tunainamisha vichwa vyetu kwa shukrani kwa Bahá’u’lláh kwamba, licha ya vikwazo kadhaa na vikali vya ulimwengu ulio katika msukosuko, Yeye amefungua milango na kurahisisha njia kwa ajili yenu—wakiwemo, kwa mara ya kwanza, wawakilishi wa Halmashauri za Kibahá’í za Kanda—kuwepo hapa katika siku hizi zisisimuazo roho.

Kipindi chenye nguvu maalum ambacho kilianza mnamo 2016 kwa miaka mia moja ya ufunuo wa Nyaraka za Mpango Mtakatifu na kilichojumuisha kumbukumbu za miaka mia mbili ya Kuzaliwa kwa Wadhihirishaji Pacha wa Mungu sasa, miaka mia moja baada ya kufariki kwa ‘Abdu’l-Bahá, inakaribia kufikia mwisho. Maendeleo ambayo jumuiya ya Kibahá’í imefanya katika kipindi hiki hayakuwa kingine zaidi kuliko yasiyo ya kawaida. Haya yamewaandaa waumini kila mahali kukidhi matakwa na kutimiza mahitaji yah atua ifuatayo ya Mpango Mtakatifu wa ‘Abdu’l-Bahá, ambao unapaswa kuanza miezi michache tu kutoka sasa na utadumu kwa miaka tisa. Uchapukaji wa anguko la utaratibu wa sasa wa kijamii, na hitaji liongezekalo kwa ajili ya michakato ya ujenzi ambayo itaongozea kwenye uibukaji wa jamii mpya ya ulimwengu, inaonekana dhahiri kila siku. Karne moja tangu Bwana kuwaachia wafuasi wa Jina Kuu Kabisa waraka ambao una mambo yenye thamani isiyo kifani kwa ajili ya ujenzi wa ustaarabu mtakatifu, tunakumbushwa juu ya maneno ya mpendwa Mlinzi: “Wajenzi bingwa wa Utaratibu uibukao wa Ulimwengu wa Bahá’u’lláh lazima wafikie vilele bora zaidi vya ushujaa kadiri jamii ya binadamu inavyozama katika vina vikubwa zaidi vya kukata tamaa, kushuka hadhi, mfarakano na fadhaa.”

Marafiki wependwa, kwenye Siku hii ya Agano sote tunatazama kwenye Kitovu chake na kukumbuka maisha na Utu wa ‘Abdu’l-Bahá, Umbo Ambalo nafsi yenyewe ilikuwa ni asili ya Agano, kile kituo cha msingi cha umoja kwa binadamu wote, kikiwaunganisha Pp moja kaumu ya watu wa dunia. ‘Abdu’l-Bahá, lile Fumbo la Mungu, “ishara ya ukuu Wake”, na “baraka kamilifu kabisa”, Ambaye amehifadhiwa katika mioyo safi ya watoto, vijana nawatu wazima wasio na idadi, hakika anatazama na akiwaongoza wependwa Wake, daima akitupia jicho la ulinzi juu yao. Katika nyakati hizi za mashaka, marafiki humgeukia ‘Abdu’l-Bahá kwa matumaini na shauku kwamba “lile kimbilio la wanadamu wote”, “ngao kwa wote walioko mbinguni na duniani”, wakitafuta msaada Wake kutoka milki za juu kadiri wanavyojitahidi kufuata mfano Wake katika njia ya huduma. Katika siku zijazo, wakati mawazo ya waumini kote ulimwenguni yamejikita juu ya “Nafsi hii takatifu na tukufu”, ninyi mnazo baraka na upendeleo wa kutoa heshima Kwake kwa niaba ya jumuiya zenu katika maeneo yale yale ambako Yeye alifanyakazi mchana na usiku kwa ajili ya utangazaji wa Hoja ya Mung una kwa ajili ya usitawi wa binadamu.

Kesho usiku, jioni ya miaka mia moja ya kufariki Kwake, tutawakumbatia mioyoni mwetu wependwa Wake kote ulimwenguni wakati tukisali katika chumba kitakatifu kilichotumiwa katika nyakati za mwisho za maisha Yake ya hapa duniani. Tutaoma kwa bidii ili ujumbe uponyao ambao 'Abdu'l-Bahá aliuishi na kujitoa dhabihu vitu Vyake vyote uweze, muda si mrefu, kupata makazi katika mioyo na roho za binadamu wote na kwamba jitihada za marafiki wa Mungu kwa suala hili ziweze kupokelewa machoni Pake.

Nyumba ya Haki ya Ulimwengu

